Viashiria vya Kitamaduni vya Maendeleo ya Binadamu: Kuelekea Kwenye Mtazamo wa Kiafrika

Dibaji 2
Utangulizi 3
Masuala na viashiria vya kupewa umbele 5
1. Utawala - uhuru wa kimawazo katika sheria na siasa 5
2. Fursa Sawa 5
3. Uhuru wa Kitamaduni 6
4. Ubunifu na ujasiriamali wa kitamaduni 7
5. Uzalishaji na usimamiaji wa maarifa 7
6. Masuala mtambuko (yenye kugusa maeneo mengi) 8
Hitimisho 9

Waraka huu uliandaliwa na:

Kikosi cha Kazi juu ya Viashiria vya Utamaduni kwa Maendeleo ya Binadamu Barani Afrika:

Dkt. Alioune Sall, Senegali (Mwenyekiti)
Dkt. Alinah Segabye, Botswana
Prof. Paul Nchoji Nkwi, Kameruni
Dkt. Fernando Dava, Msumbiji

Wakisaidiwa na:

Prof. Lupwishi Mbuyamba, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo
Zagba Oyortey, Ghana
Uta Staiger, Ujerumani

Kufuatia michango ya washiriki wa Semina ya Kimataifa juu ya Viashiria vya Utamaduni vya Maendeleo ya Binadamu Barani Afrika, Maputo, Machi 3-5, 2004:

Máté Kovács, James Sengendo, Mike Van Graan, Annamari Laaksonen, Jordi Baltà, Dr. Stephen Chifunyise*, Julia Häusermann* Osvalda Joana, Lília Momplé, Moji Okuribido-Seriki, Pierre Dandjinou, Augustin Hatar, Angeline S. Kamba, Renato Matusse, Book Sambo, Domingos Artur, Frederico Jamisse, Januário Mutaquiha, Ana Piedade A. Monteiro, Julieta Marta Álvaro Massimbe, Fátima Amade, Cardoso Tomás Muendane, Artemisa José Franco, Sérgio Armando Mangue, Boaventura Afonso, Admiro Gama Cuambe, Paulino Ricardo, Celso dos Santos Dias, Orlando Sebastião Mate, Girmay Haile, Szacay Jacques, Kassam Zahra, Mogne Severano Antuía, Pedro Cossa, Paula Morais, Nhandol Maurício Mavie

* Wajumbe wa Kikosi cha Kazi

Dibaji

Kwa muda sasa, suala la ubainishaji wa vipaumbele vya kimkakati kwa ajili ya utafiti unaofaa wa viashiria vya kitamaduni vya maendeleo vinavyokubalika duniani kote limekuwa katika ajenda za asasi nyingi. Juhudi za kuoanisha viashiria hivyo na mahitaji ya sasa ya Afrika ya upunguzaji wa umaskini, maendeleo endelevu, na uhuru wa kitamaduni zimetambuliwa na asasi kadhaa kama juhudi zenye manufaa. Asasi hizo ambazo zimekuwa zikifadhili shughuli mbalimbali zenye lengo la kufanikisha juhudi hizo ni pamoja na OCPA, the Interarts Foundation, the Forum 2004, UNESCO, na African Futures Institute (Taasisi ya Mustakabali wa Afrika).

Tangu pale juhudi hizo zilipoanza, asasi hizo zilitambua kwamba utekelezaji wake usingekuwa kazi rahisi kutokana na tofauti kubwa zilizopo katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa, nyanja ambazo ni chimbuko la utamaduni wa bara la Afrika. Aidha zilitambua kuwa mafanikio ya juhudi za namna hiyo yalitegemea kuwepo kwa uwezo wa kushirikisha utaalamu wa Kiafrika katika eneo hilo. Kwa hali hiyo, wafadhili hao walijitahidi kadri walivyoweza kuunda timu ya pamoja ya wasomi, watunga sera na watekelezaji. Manufaa ya timu hiyo yenye mchanganyiko wa taaluma na uwezo mbalimbali yalikuwa makubwa kama ilivyodhihirishwa na ubora wa uchanganuzi uliofanywa wakati wa semina mbili zilizofanyika huko Maputo katika miezi ya Machi na Agosti 2004. Naamini kwamba waraka huu ambao ni matokeo ya semina hizo utakuwa na mchango muhimu katika masuala ya uandaaji wa mipango ya maendeleo, utafiti na uhamasishaji.

UNESCO inayo fahari kuhusishwa katika kazi hii ya kikosi cha kazi, kazi ambayo ni changamoto, na inaamini kwamba matokeo yake yatakuwa mchango wenye manufaa kwa juhudi zinazofanywa sasa hivi na asasi mbalimbali duniani kote za kupingania haki za utamaduni na maendeleo ya binadamu. Kwa upande wake UNESCO itajitahidi kuhakikisha kwamba kazi hii inasambazwa vya kutosha kwa nia ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na maendeleo.

Ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Kikosi cha Kazi kwa juhudi zao, na kuwapongeza kwa mchango wao mkubwa.

Profesa Lupwishi Mbuyamba
Mshauri wa Utamaduni wa Kanda
Unesco

Utangulizi

Waraka huu umeandaliwa na Kikosi cha Kazi cha wataalamu wa Kiafrika wa utamaduni na maendeleo. Kikosi hicho kiliundwa baada ya semina ya kimataifa iliyofanyika Maputo (Msumbiji) mwezi wa Machi 2004. Lengo kuu la semina hiyo lilikuwa ni kubainisha mtazamo wa Kiafrika kuhusu viashiria vya kitamaduni vya maendeleo ya binadamu. Ukiwa umeandikwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Kongamano la Haki za Kitamaduni na Maendeleo ya Binadamu, lililofadhiliwa na Forum Barcelona, waraka huu unabainisha umuhimu mkubwa wa kutambua maeneo ya kupewa umbele na seti ya viashiria vya utamaduni vya maendeleo ya binadamu.

Mahali pa kuanzia ni kutambua muktadha wa kihistoria wa mjadala uliopo sasa kuhusu utamaduni na maendeleo katika bara la Afrika, na hasa zaidi kuhusu hali na mchakato wa kuibuka kwa dola na nguvu za soko. Jingine ni kutambua haja ya kuwa na mtazamo mpya kuhusu uraia kwa kuzingatia mjadala wa ulimwengu juu ya haki za kibinadamu na za kitamaduni katika maendeleo.

Tunatambua kwamba katika bara la Afrika dola imeibuka kupitia mikondo mbalimbali, na kwamba yapo mazingira fulani mahsusi, ambayo hayaruhusu kufanyiwa uchambuzi wa kijumlajumla. Vivyo hivyo, tumeshuhudia tofauti kubwa katika maendeleo ya uchumi na katika mtazamo kuhusu bara hili, mambo ambayo pia ni matokeo ya mazingira ya aina fulani na ambayo kwa kawaida hayahamishiki. Kwa hali hiyo, kadri tunavyojitahidi kuweka mkabala wa aina moja utakaofaa kwa bara zima, tunazingatia kuwepo kwa maeneo mahususi yenye upekee wake na ambayo yanaweza tu kuchangia katika kutoa picha ya jumla ya masuala muhimu yanayohitaji kushughulikiwa kwa ajili ya manufaa ya bara lote.

Katika miongo miwili iliyopita tumeona dola ikisailiwa, hasa kuhusu kushindwa kwake katika kutekeleza dhamana yake kwa wananchi, na tumeshuhudia, miongoni mwa mambo mengine, kuibuka na kurejea kwa aina nyingine za utambulisho, ambazo hutishia uhalali wa dola iliyopo. Katika hali ya namna hii chuki dhahiri ya dola ya sasa dhidi ya wananchi wenye vitambulisho maridhawa vya kitamaduni itakuwa ni upuuzi kwa vile wananchi wataendelea kudai haki ya kuishi kulingana na tamaduni zao na uhuru wa kuzidhihirisha kimatendo. Kutolizingatia suala hili hatimaye kutasababisha mgogoro. Hivyo, tunatambua haja ya kuwepo kwa juhudi za makusudi barani Afrika za kusimamia tofauti za kitamaduni na za kujenga mazoea ya kuheshimu haki za kibinadamu na za kitamaduni.

Maendeleo haya hayakutokea tu Afrika; hata katika mabara mengine, pale ambapo dola imetimiza wajibu wake kwa wananchi, jumuia za kiraia zimezidi kudai haki zao na kuzitaka dola zitambue tamaduni zao maridhawa, katika sura zake za kiasili na za kidiaspora (za ughaibuni au uhamishoni).

Hatua moja muhimu sana kwa bara la Afrika, bila shaka ni kuundwa kwa Umoja wa Afrika (UA) na kuongezeka kwa wito unaotaka utatuzi wa matatizo ya Afrika ufanywe na Waafrika wenyewe. Bila kujitenga na mtazamo na manufaa ya utandawazi, kama ilivyodhihirishwa na maendeleo ya NEPAD, ambayo kwa hakika husisitiza mshikamano na ushirikiano wa kikanda, maendeleo haya yanadhihirisha haja ya kubainisha uwezekano wa kukabiliana na changamoto za bara la Afrika kwa kutumia rasilimali zake yenyewe, utaalamu na nguvukazi ya watu wake, uwezo wake wa kiuchumi pamoja na urithi wake wa kitamaduni.

Ni dhahiri kwamba changamoto kubwa kwa bara la Afrika ni mwelekeo utakaochukuliwa, katika kipindi cha miaka michache ijayo, na mjadala kuhusu maendeleo na demokrasia. Hata hivyo, tayari uongozi umedhihirisha kukubali kwake utaratibu wa maongozi ya kidemokrasia, viunzi na

hati za kimataifa – kama vile Azimio la Milenia la Umoja wa Mataifa Kuhusu Uanuwai wa Utamaduni na Rasimu ya Mapatano ya UNESCO Kuhusu Uanuwai wa Utamaduni – vimeshaweka bayana kwamba wananchi hawana budi na wataendelea kujishughulisha na kupigania suala la haki za kitamaduni na maendeleo ya binadamu.

Licha ya kusisitizia haja ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya Afrika ndani ya Afrika yenyewe, ikiwa ni pamoja na kuziwezesha jumuia za kiraia za Afrika zishiriki katika masuala ya kisiasa na kiuchumi, tunatetea haja ya kuwa ni wajibu wa wadau wote duniani kutimiza majukumu yao ya kidemokrasia. Wakati ambapo masuala ya mitaji ya kijamii na utawala bora yanahusu dunia nzima, utetezi wa mambo hayo inabidi uongozwe na wadau wa utamaduni ndani ya jumuia za kiraia.

Kwa kuukiri utajiri mkubwa wa Afrika wa tamaduni mbalimbali, na kwa kuzingatia umuhimu wa haki za kitamaduni na za binadamu katika maendeleo, tunaamini kwamba mambo haya matatu hayana budi kuzingatiwa katika mikakati ya maendeleo kwa ajili ya Afrika na dunia nzima kwa jumla. Hapa ndipo tunapolibaini jukumu la ushirikiano katika ngazi za kieneo, kitaifa na kimataifa, ushirikiano wenye kuimarisha vuguvugu la kijamii na jumuia za kiraia ndani ya madola, kama njia pekee ya kuleta mafanikio. Tunaweza kuwa na picha ya Afrika inayonufaika na wataalamu pamoja na nguvukazi yake, na inayofaidi matunda ya kiuchumi kutokana na urithi na ubunifu wake wa kitamaduni, kupitia wadau na taasisi za utamaduni, hasa kwa kuweka utaratibu wa kulinda kazi za wabunifu wake. Udumishaji wa mambo haya unahitaji juhudi za pamoja za vyama vya kiraia na dola. Maendeleo endelevu yanaweza tu kuonekana endapo yataambatana na mazingira ya kufaa, mazingira yenye uwiano mzuri wa juhudi za pamoja za dola na za vyombo visivyo vya dola.

Masuala na viashiria vya kupewa umbele

1. Utawala - uhuru wa kimawazo katika sheria na siasa

Utawala ni muhimu katika kunufaika na haki za kitamaduni na za kiraia. Ushirikishaji wa wananchi katika utawala hauna budi kuwa msingi wa mkabala wa kuleta maendeleo uliojikita katika utetezi wa haki. Kwa uchache kabisa ushirikishaji wa wananchi umo katika vipengele vifuatavyo:

- Kusimamia mahusiano baina ya ngazi mbalimbali za mamlaka; kuanzia serikali ya shirikisho au serikali kuu, hadi kwenye mamlaka za mikoa na maeneo na mwingiliano baina ya ngazi mbalimbali.

  Viashiria:
  - Viunzi vya kisheria na uingizaji wa viunzi vya kimataifa katika mazingira ya ngazi ya taifa na ya eneo.
  - Uwezo wa kuhakikisha utawala shirikishi kwa kuzingatia dira ya pamoja
  - Uhusiano baina ya dola na mwananchi, baina ya soko na mwananchi, baina ya soko na dola.

- Kusimamia uanuwai wa utamaduni, ukiwemo ukabila, katika hatua ya kutoa haki kwa wananchi

  Kiashiria:
  - Sera jumuishi, uingizaji wa sera za utamaduni katika maendeleo

- Kusimamia mifumo tofautitofauti ya sheria, kwa mfano kutumika pamoja kwa mifumo ya sheria za kijadi na za kisasa katika nchi moja, katika hali ambayo inalinda haki za kitamaduni na za kibinadamu na kusimamia uwajibikaji na utabirikaji.

  Kiashiria:
  - Uanzishaji na usimamiaji wa ubia (ubia baina ya sekta binafsi na ya umma, ngazi mbalimbali za mamlaka n.k.)

2. Fursa Sawa

Umaskini ni moja ya changamoto kubwa katika maendeleo: husababisha ubaguzi wa kijamii, kupoteza uwezo na haki za kiraia. Mara nyingi huhusishwa na kukosekana kwa usawa katika upatikanaji na usambazaji wa:

- Rasilimali za kuzalishia, kama vile misitu, kilimo, uvuvi, fedha n.k; matumizi ya rasilimali hizi sharti yatawaliwe na nia ya kutoa fursa sawa na kuongeza nafasi za ajira, za kujiajiri kwenye manufaa, na za kujenga ujasiriamali.

  Viashiria:
  - Mageuzi ya mifumo ya kumiliki ardhi
  - Uwazi katika upangaji wa bajeti na ukusanyaji wa mapato
  - Programu za uwekezaji wa umma
  - Utoaji wa mikopo
  - Upatikanaji wa ajira

- Huduma za kijamii: elimu, afya na habari

  Viashiria:

- Ugatuaji wa miundombinu
- Uwepo wa rasilimali zinazomilikiwa na jamii
- Uandikishaji watoto shuleni na ujuzi wa kusoma na kuandika
- Huduma za afya ya uzazi na ngono
- Huduma za afya
- Huduma za nyumba
- Kuwapatia walemavu nafasi ya kunufaika na haki zao za utamaduni
- Kuthamini na kulinda Haki Miliki za Kazi za Kitaaluma
- Kuthamini, kulinda na kutumia Mifumo ya Maarifa ya Wenyeji

o Asasi zinazowajibika kwa wananchi

Viashiria:

- Kuwako kwa mazingira na viunzi vya kisheria vinavyowezesha kuanzisha asasi zisizo za kiserikali (AZISE) na jumuia za kijamii
- Viunzi vya kisera vinavyoruhusu kufanya kazi kwa kushirikiana na ngazi ya serikali
- Asasi za kiuchumi kwa ajili ya wakuzaji na wataalamu wa masuala ya utamaduni
- Vyama vya kitaalamu

3. Uhuru wa Kitamaduni

Uhuru wa kitamaduni ni muhimu katika kujenga na kudumisha mazingira yenye kuleta uvumilivu na heshima kwa tofauti za kitamaduni na kuhakikisha kutumika kwa njia mbalimbali za kujitambulisha kitamaduni Maeneo muhimu ambayo yatahitaji kutazamwa vizuri na watunga sera pamoja na watendaji wa utamaduni ni pamoja na:

o Wingi wa lugha

Viashiria:

- Uchunguzi na uhifadhi wa lugha za wachache na zile zilizo hatarini kutoweka.
- Uanzishaji wa vyombo vya habari vya jumuia kwa lugha za wenyeji
- Urasimishaji wa lugha asilia za taifa.

o Elimu kwa lugha ya kwanza (lugha ya mama)

Viashiria:

- Uandishi wa vitabu vya kielimu na vya kujiburudisha
- Sera zinazohusu ufundishaji wa lugha na matumizi yake shuleni.

o Kupitia upya mitaala ili kuimarisha uanuwai wa kitamaduni

Viashiria:

- Mitaala iliyorekebishwa katika ngazi zote, na yenye kuingiza elimu ya utamaduni

o Uhuru wa kidini, haki za kitamaduni

Viashiria:

- Kutobagua na kuzitambua sikukuu za umma
- Kulinda asasi za kidini na maeneo ya ibada
- Kuwepo kwa uanuwai wa dini shuleni

o Utambulisho maridhawa

Viashiria:

- Utetezi wa jamii asilia za watu wachache
- Ulinzi wa vielezo vya kitamaduni, kwa mfano, shughuli za miviga
- Kukataza aina zote za ubaguzi
- Kujenga utamaduni wa kuvumiliana kwa njia ya vifaa vya kielimu

4. Ubunifu na ujasiriamali wa kitamaduni

Kuimarisha uvumbuzi na ubunifu kwa kutoa rasilimali na kuanzisha asasi mbalimbali za kuwasaidia wadau, na kwa kujenga mazingira yanayofaa kwa ajili ya uanzishaji wa miradi ya kitamaduni.

o Masoko ya bidhaa za utamaduni na ulinzi wa wazalishaji na rasilimali

Viashiria:

- Ufadhili wa maonyesho na matamasha kwa ajili ya wasanii na wanautamaduni
- Uwekezaji wa sekta mbalimbali katika sekta za sanaa na urithi wa kitamaduni
- Rasilimali za fedha kwa ajili ya kusaidia ujasiriamali wa kitamaduni, kama vile huduma za mikopo
- Uundaji wa mifuko ya kufadhili sanaa kitaifa na kikanda
- Ulinzi wa Haki Miliki ya kazi za Kitaaluma na nyingine za hataza
- Ushiriki na ugawanyaji wa rasilimali zinazotokana na utalii wa kiutamaduni
- Uchangiaji wa tasnia ya utamaduni katika Jumla ya Pato la Taifa

5. Uzalishaji na usimamiaji wa maarifa

Msingi wa uwezeshwaji wa jumuia za kiraia ni uboreshaji wa uzalishaji na usimamiaji wa maarifa ya jumla na yale ya kitaalamu, pamoja na matunda ya maarifa hayo.

o Utafiti

Viashiria:

- Orodha za shughuli na sera za utamaduni
- Hifadhi data za bidhaa na wataalamu wa utamaduni
- Ubainishaji wa vigezo vya mila na desturi zifaazo
- Uthibitishaji wa ubora

o Ugharamiaji

Viashiria:

- Ugharamiaji wa shughuli za utafiti, ASIZE na za mashirika ya kijamii
- Msaada wa kifedha kwa asasi, Elimu ya Juu

o Uendelezaji na uhifadhi wa rasilimali zitokanazo na maarifa, zikiwemo amali za urithi

Viashiria:

- Kufadhili shughuli za makumbusho na rasilimali rithiwa
- Kuimarisha asasi za nyaraka na uhifadhi
- Kufadhili vituo vya kijamii vya amali rithiwa na suhula za taarifa na huduma
- Kuhifadhi urithi batini (uliofichika), kama vile mapokeo simulizi

o Njia na mbinu

Viashiria:

- Kuanzisha vifaa na vigezo vya kutathimini taathira ya maendeleo ya kitamaduni

- Kuanzisha faharasa
- Kuanzisha utaratibu wa kusimamia sanaa

o Hati, Machapisho, Usambazaji

Viashiria:

- Uanzishaji na usaidiaji wa maktaba za umma
- Uhimizaji wa utamaduni wa kujisomoea
- Kusaidia biashara ya wachapishaji wenyeji
- Teknolojia ya habari na mawasiliano na tovuti
- Utumiaji kikamilifu wa amali hai, k.m. wazee, wahifadhi wa mapokeo simulizi
- Ubadilishanaji wa maarifa yaliyopo, hasa yale yenye manufaa
- Kuheshimu uhuru wa habari
- Kurekebisha uamuai wa habari mbalimbali katika vyombo vya habari ndani ya nchi

6. Masuala mtambuko (yenye kugusa maeneo mengi)

Maendeleo ya binadamu yanahusu uboreshaji wa kile kilichochaguliwa na watu. Kujenga uwezo wa mtu binafsi na wa jumuia kunaweza kuchangia katika uboreshaji wa uwezo wao wa kujiendeleza. Kwa upande mwingine ukosefu wa fursa sawa na wa usawa kijinsia unaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya binadamu. Kwa mwelekeo huohuo, UKIMWI katika Afrika na hata mahali pengine ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo. Kwa hiyo, inaaminika kwamba kuzungumzia masuala haya kwa utaratibu unaoeleweka ndiyo njia ya kufanikisha katika maeneo ya aula (kipaumbele), na viashiria vya utamaduni vilivyobainishwa hapo juu.

o Kujenga uwezo

- Michakato na rasilimali za kiasasi
- Maendeleo ya Rasilimali-watu, mf. wanautamaduni, na wasimamizi
- Rasilimali Fedha
- Ubadilishanaji wa miundo mbinu na ujenzi wa Mtandao katika ngazi za taifa, kanda, na miongoni mwa serikali

o Jinsia

- Elimu ya jinsia
- Uundaji wa sera za jinsia na uingizaji wa masuala ya jinsia katika nyanja zote
- Elimu kwa watoto wa kike
- Utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali na wanautamaduni wanawake
- Kufuatilia habari za kijinsia katika vyombo vya habari
- Idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi
- Tathmini ya taathira ya jinsia

o VVU/ UKIMWI

- Sera za VVU/UKIMWI na programu za mahali pa kazi katika ngazi ya eneo na taifa
- Ushirikishaji wa jamii katika kubuni programu za kuzuia , kutibu na kuhudumia wagonjwa
- Kujitolea kwa uongozi katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI
- Kufuatilia athari za VVU/UKIMWI katika sekta ya utamaduni
- Kushughulikia masuala ya unyanyapaa na ubaguzi
- Programu za masuala ya jinsia kuhusiana na VVU/UKIMWI

Hitimisho

Kukuza maendeleo ya binadamu na kuheshimu tofauti za kiutamaduni ni changamoto kubwa kwa Afrika na kwa dunia nzima. Katika mazingira ya sasa mambo matatu ni muhimu katika kufanikisha lengo hili.

La kwanza ni kubuni rajua (dira) ya pamoja: Afrika haina budi kubainisha rajua yake yenyewe kwa ajili ya mustakabali wake. Tafiti za malengo ya muda mrefu zilizofanyika katika ngazi ya kitaifa na kikanda zinaonyesha kwamba rajua ya namna hiyo itajumuisha nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kimazingira, kitamaduni na kiteknolojia. Katika kila uwanja, mikakati sahihi haina budi kubuniwa kwa kuoanishwa na malengo ya muda mrefu ya rajua hiyo. Katika uwanja wa utamaduni, mkakati unaofaa zaidi ni wa ukuzaji wa umoja katika uanuwai kama unavyohimizwa na Ripoti ya UNDP[1] 2004 ya Maendeleo ya Binadamu. Mkakati huu hautilii tu mkazo katika kuvumiliana, bali pia katika kushirikiana miongoni mwa vikundi vya wenyeji katika ngazi ya kitaifa na ya kikanda. Aidha unadokeza haja ya kuvumiliana na kushirikiana katika ngazi ya kimataifa miongoni mwa mataifa.

Mchakato wa uundaji wa rajua hiyo hauna budi kupewa umuhimu sawa na matokeo yake. Mchakato huo hauna budi kuwa shirikishi na jumuishi kwa kadri iwezekanavyo, kama lengo ni kuwa na rajua yenye kunufaisha wengi na inayomilikiwa na walio wengi pamoja na jumuia mbalimbali.

Pili, utendaji ni kipengele muhimu na unapaswa uhusishe masuala ya shughuli za utafiti, hatua za kisera na shughuli za utekelezaji. Shughuli za utafiti hazina budi kushughulikia masuala ya viashiria vya kitamaduni vya maendeleo na viashiria vya maendeleo ya kiutamaduni. Masuala ya kisera yatahusu uundaji na utekelezaji wa viunzi ambavyo vitalazimisha kuwapo kwa tathimini ya ubora wa shughuli za utamaduni. Shughuli za utekelezaji hazina budi kuelekezwa katika kuhimiza kuingiza sera za utamaduni katika mikakati, sera na programu za maendeleo za maeneo na za taifa.

Tatu ni tathmini na ufuatiliaji. Hata kama rajua iliyobuniwa itakuwa inatia hamasa na utekelezaji wake utafanywa vyema, bado maendeleo haya inabidi yatazamwe kama mchakato wa kujifunza ambao unapaswa kufanyiwa mapitio, marekebisho, na mageuzi ya mara kwa mara. Na ni muhimu kuhakikisha kwamba wadau wote wanashirikishwa katika mchakato huu wa tathmini na ufuatiliaji, na kwamba juhudi za makusudi zinachukuliwa kuhakikisha kwamba wote wanashirikishwa kikamilifu.

[1] UNDP – Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa